

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI**



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ijumaa, 01 Disemba 2023


**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MHESHIMIWA DKT. SAMIA
SULUHU HASSAN, KUFUNGUA MKUTANO WA KWANZA WA KITAIFA WA DIRA
YA MAENDELEO YA TAIFA**

1. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, atafungua Mkutano wa Kwanza wa Kitaifa wa Dira ya Maendeleo ya Taifa utakaofanyika siku ya Jumamosi, tarehe 09 Disemba 2023 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam. Lengo kuu la Mkutano huu ni kuzindua, kupokea na kujadili taarifa ya kitafiti ya Tathimini ya Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.
2. Taarifa ya kitafiti ya Tathimini ya Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, pamoja na mambo mengine, imeainisha mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Dira ya kwanza ya Taifa ya Maendeleo. Dira hii ilianza kutekelezwa mwaka 2000 na itafikia mwisho wake mwaka 2025. Pamoja na mafanikio mengine, taarifa ya tathimini inaonesha kuwa pato la mtanzania (GDP per capital income) limeongezeka kutoka dola za kimarekani 399.5 (TZS 322,597) mwaka 2000 hadi kufikia dola za kimarekani 1,200 (TZS 2,880,000) mwaka 2022. Aidha, Tanzania imefikia asilimia 124 ya kujitoleza kwa chakula ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 140 ifikapo mwaka 2025. Hatua hii imewezesha Tanzania kukabiliana na njaa kwa mikoa na wilaya zote nchini. Mtandao wa barabara za lami na zege (paved roads) katika mikoa umeongezeka kutoka KM 4,179 mwaka 2000 hadi kufikia KM 11,966.38 mwaka 2023. Mafanikio mengine ni pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka vifo 760 kwa vizai hai 100,000 mwaka 2000 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2022, ikiwa tumevuka

lengo la kufikia vifo 265 ifikapo mwaka 2025. Matokeo kamili ya tathimini hii yatatolewa siku ya Mkutano.

3. Aidha, katika Mkutano huu, Mheshimiwa Rais atazindua rasmi Timu Kuu ya Kitaalam ya Dira (***National Vision Core Technical Team***) na Kamati ya Usimamizi wa Dira (***National Vision Steering Committee***), pamoja na nyenzo za kidigitali zitakazotumika katika kukusanya maoni ya wadau.
4. Kwa kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba zoezi la kuandaa dira mpya ya maendeleo liwe jumuiishi na shirikishi, mkutano huu utahudhuriwa na wadau mbalimbali kutoka pande zote za nchi yetu. Wadau hawa ni pamoja na viongozi wakuu wa serikali ya muungano na serikali ya Zanzibar, mawaziri na makatibu wakuu, wakuu wa mikoa, viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa taasisi za dini, viongozi wa taasisi mbalimbali za sekta binafsi, viongozi wa makundi mbalimbali ya kijamii, yakiwemo wazee, watu wenye ulemavu, wakulima, wafugaji, wavuvi na wachimbaji madini, jumuiya za kimataifa, wasomi, waandishi wa Habari, n.k. Jumla ya wadau 971 wamealikwa kushiriki katika mkutano huu.
5. Wananchi wanaombwa na kusisitizwa kufuatilia mchakato wa kuandaa Dira mpya na kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yao kuhusu Tanzania waitakayo katika miaka ijayo.
6. Kwa kuwa Mkutano huu unafanyika siku ya Uhuru, Mheshimiwa Rais anatarajiwa kutumia siku hii kutoa ujumbe maalum katika kuadhimisha miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Imetolewa na



Kitila Alexander Mkumbo (Mb.)

WAZIRI WA NCHI

OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

Dar es Salaam, 01 Disemba 2023.

Kwa mawasiliano na taarifa zaidi:

Immaculate Makilika

Simu: 0717 029026

Email: immaculate.makilika@planning.investment.go.tz